# MIMI NASEMA NITAENDELEA MBELE.

LUKA 22:28-30, YAKOBO 1:2, ZABURI 41:1-7.

# JUNE 2013

*NA.Sambaya Edmund C(SEC).*
*Parokia ya Lowerere'*
*Usseri Rombo-Jimbo kuu la Moshi.*
*Call:0759564088/0783868793.*




2.Mnaocheka shida zangu ole wenu(mimi nasema),
Ninawaomba tulieni Mungu yupo(milele yote),
Namshukuru alieniumba mimi(Mtazame)Tazama.....
3.Hakuna jambo wewe unalomiliki{ulionayo},
Ni yake Mungu amekupa mshukuru{tazama we},
Usijigambe kwani hayo yatakwisha{mtazame}..........
4.Walo na shida mbalimbali saidia[ee ndugu yangu]
Walo na shida mbalimbali wapokee[usiwaache]
Usiwatupe kwani Mungu ni mpaji[mambo yote].........
5.Walo na shida wakikupigia simu (tazama wewe)
Haupokei unaacha inakata(we ndugu yangu)
tena pokea sikiliza saidia(Mungu yupo)..........

6.Mungu kaumba watu wote sio sawa{tazama hawa}
Kuna yatima walemavu na wajane{tazama hawa}
Na wkimbizi wenye njaa masikini{nae baba}.........
7.Tazama wewe umepewa nae Mungu[na sio kwamba]
Ni kwa uweza wako wewe peke yako[ee ndugu yangu]
ni Mungu baba amekupa saidia[tena ona]..........
8.Usidharau ndugu yangu sikiliza(yeyote yule)
Kwani ye Mungu aloumba anajua(alivyoumba)
Vyo vitu vyote kaviumba kwa kusudi(tazama we)........
9Nina kemea roho chafu za shetani[nazo zishindwe]
Ushirikina na mambo yote ya Giza[nayo yashindwe]
Ee Mungu baba nishushie nguvu zako[nisishindwe].........

10.Na ufisadi siku zote twakemea(tena sikia)Na rushwa
zote ndugu yzangu kemeeni(milele yote)Ishini kama ndugu wa jamii moja(mile--le)..........

**Edmund Sambaya**